# Marking Scheme KCSE 2016

## *102/2 LUGHA*

### *UFAHAMU*

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali*

*Ulimwengu unatakiwa kuzua mbinu za kulitatua tatizo la ufukara ambao ni kikwazo kikuu cha juhudi za maendeleo. Ufukara unayakabili mataifa mengi yanayoendelea na kuyatosa kwenye shida nyingi huku mataifa ya magharibi yakizidi kupiga hatua kubwa za kimaendeleo. Tofauti iliyopo kati ya mataifa yanayoendelea na yaliyoendelea inaendeiea kuongezeka kila siku.*

*Miongoni mwa sababu zinazochangia katika ufukara huu ni pamoja na ufisadi, uongozi mbaya, turathi za kikoloni na uchumi unaotegemea kilimo ambacho hutegemea mvua isiyoweza kutabirika. Vilevile, mataifa yanayoendelea yana idadi kubwa ya watu inayoupiku uwezo wa mataifa husika. Pamoja na haya, mataifa haya hayana uwezo wa kuwakomboa raia wake kutoka katika lindi la umaskini huu unaokithiri. Ukosefu wa elimu na nafasi adimu za kazi huchangia pia katika tatizo hili. Ni wazi kuwa ufukara una athari hasi kote ulimwenguni. Aghalabu, ufukara huchipuza matendo mabaya. Ni rahisi kuwashawishi wananchi maskini kushiriki katika uhalifu iii kujinasua kutoka kwenye lindi la kimaskini. Udhaifu huu huweza kuzaa mbegu ya kuatika maovu ya kila aina ukiwemo ugaidi. Mataifa yaliyoendelea yanatakiwa kuyaburai madeni yanayoyadai mataifa yanayoendelea kama njia moja ya kupambana na ufukara. Mataifa haya maskini hutumia asilimia kubwa ya mapato ya kitaifa kuyalipia madeni haya. Hali hii imeyafanya mataifa haya kushindwa kujikwamua kutoka kwenye minyororo ya ufukara. Njia nyingine ya kuyasaidia mataifa haya ni kukubali kutoa ruzuku za kimaendeleo badala ya mikopo kwa nchi husika.*

*Mataifa yanayoendelea nayo yanatakiwa kuchukua hatua katika kuwanusuru raia wake kutoka kwenye dhiki hii.Ni sharti yaibuke na mikakati kabambe ya kupambana na ufukara. Itakuwa na faida kubwa iwapo mataifa haya yataunda sera zinazotambua ufukara kama tatizo kuu linalozikabili na kuweka mikakati ya kuwaokoa raia wake kutoka kwenye tatizo hili. Pamoja na mikakati hii ni kuzalisha nafasi za kazi, kuimarisha miundo msingi,kuendeleza elimu inayolenga kutatua matatizo maalumu katika jamii na kupanua viwanda. Kuna pia haja ya viongozi kuwa waangalifu ili mfumo wa soko huru ambao unaendelezwa na mataifa yaliyoendelea usiishie kuwa chanzo cha kufa kwa viwanda asilia. Maamuzi yote ya sera za kiuchumi sharti yauzlngatie uhalisia wa maisha ya raia wa mataifa haya.*

**(a) Eleza athari za madeni kwa nchi zinazoendelea.(alama 2)**

- *Asilimia kubwa ya patu la mataifa yanayoendelea huishia kulipa madeni haya.*
- *Hivyo inakuwa vigumu kwa mataifa hayo hujikwamua kutokana na umaskini.*

**(b) Kwa nini umaskini unatawala mataifa yanayoendelea? (alama 4)**

- *Ufisadi, uongozi mbaya, turathi za kikoloni, uchumi kutegemea kilimo chenye mvua isiyotabirika, idadi kubwa ya watu, nafasi adimu za kazi, madeni na ukosefu wa elimu*

**(c) Mwandishi anatoa mapendekezo yapi kwa mataifa yanayoendelea katika kutatua tatizo la ufukara?(alama 4)**

- *Kuibuka na mikakati bora ya kupambana na umaskini.*
- *Sera zinazotambua kuwa raia wake wengi ni maskini.*
- *Kuzalisha nafasi za ajira kuimarisha miundo msingi.*
- *Kuendeleza elimu inayolenga kutatua matatizo maalum*
- *Kupanua viwanda.*
- *Kuhakikisha kuwa mfumo wa soko huu hauishii kusababisha kufungwa kwa viwanda.*

**(d) Mfumo wa soko huru una mathara gani kwa mataifa yanayoendelea? (alama 2)**

- *Unaweza kuwa chanzo cha kufa kwa viwanda asilia.*

**(e) Taja visawe vya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika kifungu. {alama 3)**

***(i)Turathi za kikoloni***

- *Masalio ya kikoioni/ukoloni mambo Ieo / athari za ukoloni.*

***(ii) Kuatika***

- *Kuzalisha/kuwa*
- *chanzo/kuanzisha/kuleta/kusababisha/kupanda.*

***(iii) Kuyaburai***

- *Kuyasarnehe/kuyaondoa/kuyasahau/kuyapuuza/kuyafutilia mbali*

# *MUHTASARI*

## *2016*

## *MUHTASARI (alama 15)*

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

*Taifa huundwa na watu wanaoishi katika nchi moja na wanaojitambua kisiasa kama watu walio na mwelekeo, maono na hatima sawa. Utaifa hujengwa kwenye misingi ya mapenzi kwa nchi, Utambuzi wa cheo, eneo, hadhi, rangi na hata makabila wanakotoka raia wa taifa moja si chanzo cha kuwatanganisha. Nchi moja huweza kuundwa na watu walio na tofauti chungu nzima zikiwemo tofauti za kikabila, kitabaka na kimawazo. Hata hivyo, watu hao huwa na folsafa na imani sawa kama taifa inayoashiriwa hasa na wimbo wa taifa. Hata hivyo haya yotc hayawezi kuwafikia katika kiwango cha kuunda taifa. Uzalendo ndio mhimili mkuu wa utaifa. Uzalendo ni mapenzi aliyo nayo mtu kwa nchi yake. Mapenzi haya humwongoza mtu katika mawazo yake, itikadi yake, matendo yake, matamanio yake na mkabala wake kuhusu nchi na hatima ya nchi yake.*

*Mzalendo hawezi kushiriki katika matendo yanayoweza kuiletea nchi yake maangamizo kwa vyovyote vile. Mzalendo huongozwa na mwenge wa wema. Mzalendo hawezi kushiriki kwenye shughuli zozote zinazohujumu mshikamano wa kitaifa. Yeye hatawaliwi na ubinafsi wa kutaka kufaidi nafsi yake naya jamii yake finyu. Matendo yake yote huongozwa na ari ya kuiboresha nchi yake. Anayeipenda nchi yake hujiepusha na ulafi wa kujilimbikizia mali. Yuko radhi kuhasirika mradi taifa lake linufaike.*

*Utaifa ni mche aali unaopaliliwa kwa uzalendo, kuepuka uchu wa nafsi na taasubi hasi zikuwepo za kikabila na ubinafsi. Hali hii inapofikiwa, hatima ya taifa na mustakabali wa raia wake huwa wenye matumaini makubwa.*

(*a*) **Kwa maneno 40 - 50 dondoa sifa kuu za utaifa.(alama 6, 1 ya mtiririko)**

- *Kuwepo kwa hatima sawa*
- *Kuwepo kwa maono sawa*
- *Kuwepo kwa falsafa/imani/itikadi sawa.*
- *Kuwepo kwa mwelekeo mmoja.*
- *Umejengwa kwa hisia za mapenzi kwa nchi.*

**(b) Ni nini misingi ya kutathmini mzalendo? (maneno 60 - 70) (alama 9, 1 ya mtiririko)**

- *Hawezi kushiriki kwenye shughuii zozote zinazohujumu mshikamano wa kitaifa.*
- *Hawezi kutawaliwa na ubinafsi*
- *Hujiepusha na ulafi wa kujilimbikizia mali.*
- *hawezi kutenda mambo ya kuiletea nchi yakemaangamizo.*
- *Yuko radhi kuhasirika kwa manufaa ya taifa lake.*
- *Matendo yake huongozwa na mwenge wa wema.*
- *Matendo yake huongozwa na ari kuiboresha nchi yake.*

## *3.MATUMIZI YA LUGHA*

### *3. MATUMIZI YA LUGHA (alama 40)*

**(a) Tumia nomino yoyote katika ngeli ya 1-1 kutunga sentensi. (alama 1)**

- *Mfano wa nomino ni kama: chumvi, sukari, mvua, chai, asali, furaha, huzuni, petrol nk. Mfano wa sentensi: Chumvi imemwagika.*

**(b) (i) Nini maana ya silabi (alama 2)**

- *Ni sauti moja au zaidi zinazotamkiwa kama fungu moja la sauti.*
- *Silabi ni kipashio cha utamkaji ambacho hutumiwa kwa pamoja kama fungu moja la sauti.*
- *Tamko, pigo, tamshi.*

***(ii) Tunga neno lenye muundo huu wa silabi:***
***Irabu + konsonanti + konsonanti + irabu***

- *afya, anza, ibia, enda, unga, uzwa, igwa,ugwa.*

**(c) Tunga sentensi hii upya kwa kufuata maagizo: Wasichana wanaingia darasani kwa haraka (andika kinume chake) (alama 2)**

- *Wasichana wanatoka darasani polepole/taratibu/ asteaste/ halahala/ala ala.*

**(d) Tambua kiambishi awaii na tamati kati neno: Alalaye (alama 2)**

- *A - awali*
- *a - ye – tamati*

**(e) Ainisha vivumishi katika sentensi hii: mzee mwenyewe ni mkongwe na amepewa zawadi kwa kuwa shamba lake lilitoa mazao mengi. (alama 4)**

- *Mwenyewe - kivumishi cha pekee Mkengwe - kivumishi cha sifa Lake - kivumishi kimilikishi Mengi - kivumishi cha idadi*


**(f) Askari wasipopiga doria wala kushikiana na raia hawatakuwa wametuhakikishia usalama. (yakinisha sentensi hii) (alama 2)**

- *Askari wakipiga/wanapopiga/ wapigapo/ watakapopiga doria na kushirikiana na raia watakuwa wametuhakishia usalama.*

**(g) "Shughuli yetu itakamilika kesho", mama alimwambia mwanaye Juma. (Andika katika usemi wa taarifa). (alama 2)**

- *Mama alimwambia mwanawe/mwanaye Juma kuwa shughuli yao ingekamilika siku ambayo ingefuata.*

**(h) Changamua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha matawi. Mpria ulichezwa tulipokuwa tukipika.(alama 3)**



**(i) Dhihirisha matumizi matatu tofauti ya kimaana yatakayotokea ketenzi "ona" kikinyambuliwa katika kirai hiki "ona ndoto". (alama 3)**

- *Onea ndoto*
- *Onewa ndoto*
- *Oneshwa ndoto*
- *Onesha ndoto*
- Onoana ndoto

**(j) Eleza matumizi ya hali za "ka" na "hu" katika sentensi zifuatazo:**
**(i) Balozi huja hapa kila mara. (alama 1)**

- *Hali ya mazoca kila mara kila siku mara kwa mara*

**(ii) Mpishi alipika, akapakuwa na akagawa chakula. (alama 1)**

- *vitendo vinafuatana Mfulultzo wa vitendo Mfuatano wa vitendo Kufululizwa kwa vitendo*

**(k) Eleza maana mbili zinazojitokeza katika sentensi: Tuiiitwa na baba. Mtendaji ni baba**

- *Mtu mwingine alituita mimi pamoja na baba. Sisi pamoja na baba*
- *Mimi na mtu mwingine tuliitwa na baba Mimi na watu wengine tuliitwa na baba.*

**(I) Akifisha: Shangazi alimwambia mwanawe njoo nikupcleke kwenu jioni mtoto aliuliza kwetu wapi?(alama 4)**

- *Shangazi alimwambia mwanavve, "Njoo nikupeleke kwenu jioni." "Mtoto aiiuliza, "Kwetu wapi?"*

**(m) Eleza matumizi mawili ya kiambishi -ji-.(alama 2)**

- *Mwanzoni mwa baadhi ya nomino katika ngeli ya LI-YA.*
- *Kujirejeiea/kircjeshi cha mtenda/ kujitendea.*
- *Kuonyesha uzoefu*
- *Kuonyesha ukubwa Kuonesha udogo/udunishaji.*

**(n) Tunga sentensi hii upya kwa kutumia visawe vya maneno yaliopigwa mstari. Kiambaza kilimuumiza ghulamu alipokuwa akipanda. (alama 3)**

- *Ukuta ulimuumiza mvulana alipokuwa akiuparaga*

**(o) Tumia kitenzi "Fa" katika sentensi kuonyesha mazoea. (alama 2)**

- *Hufa/hufisha/afaye/wafao*

**(p) Ainisha vihusishi katika sentensi ifuatayo: Babu alifika mapema kuliko wote halafu akaondoka.(alama 2)**

- *Kuliko - kulinganishi/kiwango Halafu - wakati.*

**(q) Tumia kitenzi "tafakaru" kama nomino katika sentensi. (alama 1)**

- *Kutafakari kwake kulimnufaisha.*
- *Utafakari huo utamwezesha kupiga hatua kimaendeleo.*
- *Tafakari zao ndizo zimewafikisha walipo.*

**(r) Andika upya sentensi ifuatayo kwa kutumia viwakilishi badala ya nomino zilizopigwa mstari. Mwanamziki ataembelea mji. (alama 1)**

- *Yeye/yule/huyu/huyo atatembelea mji.*

## *ISIMU JAMII (alama 10)*

**Kwa kutoa mifano maridhawa, eleza kaida zozote tano ambazo matumizi ya lugha hutegemea katika jamii.**

- *Mazingira/ mahali*
- *Jinsia/uana*
- *Cheo/hadhi*
- *Umri*
- *Mada*
- *Muktadha*
- *Wakati/misimu*
- *Malezi*
- *Taaluma/kazi/shughuli*
- *Mila/desturi/u'amaduni*
- *Hadhira.*
- *Njia ya mawasiliano I mani/dini/itikadi*
- *Tajriba/uzoefu/ujuzi*
- *Elimu(kiwango cha elimu)*
- *Hali/hisia*
- *Lugha azijuazo mtu*
- *Wahusika*
- *Uhusiano*
- *Madhumuni/lengo/nia*
- *Tabaka*
- *Falsafa/mtazamo*

# *102/3 FASIHI*

**SEHEMU B: RIWAYA**

**K. Walibora:** *Kidagaa Kimemwozea*

*Jibu swali la 2 an la 3*

***2. Fafanua mjukumu ya elimu na dini katika jamii kwa mujibu wa riwaya: Kidagaa Kimemwozea.*** **(Alama 20)**

- *Elimu inasaidia kuelezea hisia za mtu kupitia maandishi. Mfano - Amani ameandika mswada kuonyesha msimamo wake katika masuala tofautiElimu iliyosisitizwa ni elimu ya kujielewa. Elimu ya kujua mtu atoka wapi na anaelekea wapi kwa mujibu wa Amani. Elimu imesawiriwa kuwa muhimu licha ya utajiri na kutosheka maishani. Baada ya muda mrefu, Amani anarudi chuoni na kupata shahada ya kwanza katika Fasihi na Falsafa. Elimu ni njia ya kujipatia heshima na umaarufu. Nasaba Bora alimheshimu ndugu yake kwa uwezo wake katika lugha. Hakupenda wakati ambapo inamlazimu kusoma hotuba kwa kiingereza asichokielewa*
- *Wasio na elimu wanabaki kutaabika. Mfano Chwechwe Makweche baada ya kuacha masomo katika darasa la saba na kuwa mchezaji shupavu, analemewa na maisha baada ya kuvunjika pfupaja la mguu.*
- *Elimu imetumiwa kama chombo cha kuwakweza baadhi ya raia katika madaraka - kama Majisifu anapata kazi kutokana na elimu yake.*
- *Elimu pia imetumiwa kama chombo cha mapinduzi kwa kutetea haki za wanyonge. Mfano - Madhubuti anapomaliza masomo yak Urusi anaungana na Amani kuleta mabadiliko Sokomoko.*
- *Imani katika dini inajitokeza ambapo kila linapojitokeza jambo mbaya watu hukimbilia dini.*
- *Kwa upande mwingine dini imebainishwa kama chombo cha kuadilisha. Mfano: babake Nasaba Bora na Majisifu aliwalea kwa mwongozo wa bibilia huku akiwasihi waishi kwa umoja na upendo.*
- *Dini pia huweza kutumiwa kama hifadhi ya maovu. Kwa mujibu wa Majisifu maovu mengi kama vile mauaji hufanywa katika jina la Mungu kutokana na unafiki. Dini ina jukumu la kuwapoza wanaomboleza. - Dini imetekeleza jukumu la kuunganisha familia pamoja mfano: Babake Nasaba Bora alihakikisha familia yake imeunganishwa na dini.*

***3. "Wasemao husema, atamtaye hachoki."***

- *Haya ni maneno ya msirmulizi yanamhusu:*

**(a) Fafanua muktadha wa dondoo hili. (Alama 4)**

- *Majuhuni aliyejitahidi kumfurahisha mpenziwe Mitchelle aliyekuwa amekataa kuolewa naye mpaka ajenge jumba la kifahari. Licha ya jitihada zake Majununi, Mitchelle alikataa kuolewa na Majununi na baadaye Maajununi akaamua kutooa kamwe.*

**(b) Kauli hii ina tnaana gani kwa mujibu wa muktadha huu. (Alama 2)**

- *Majununi hakufa moyo katika harakati za kutaka kumwoa Mitchelle. Alijitahidi kutimiza matakwa ya mpeni wake kwa kujenga nyumba nyingine.*

**(c) Jadili umuhimu wa kinachotafutwa katika riwaya ya Kidagaa Kimemwozea. (Alama 14)**

- *Imani anatafuta haki ya kunyimwa malezi ya wazazi wake waliouliwa kinyama. Imani anatafuta haki ya familia yake iliyonyanganywa shamba lao.*
- *Amani anatafuta haki ya Ami yake Yusufu.*
- *DJ anatafuta haki baada ya kushambuliwa na jibwa lake Nasaba Bora.*
- *Amani anatafuta haki ya mswada uiiokataliwa na wachapishaji na baadaye kuchapishwa kwa jina la mtu mwingine.*
- *Chwechwe Makweche anatafuta haki ya kuumia michezoni bila kufidiwa.*
- *Watoto wa Majisifu wanalilia haki ya kuishi kama binadamu wengine licha ya ulemavu wao. Amani anatafuta haki ya kudhulumiwa na mtemi Nasaba Bora kwa kizingizio kuwa alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na Mkewe Bi Zuhura. Amani atafuta haki ya kujua waliokuwa wazazi wa kitoto Uhuru baada ya yeye kulazimishwa kukilea licha ya kuwa hakuwa babake. Amani na Imani wanatafuta haki ya kufungwa kwa kizingizio kuwa walimwuua mtoto Uhuru. Wanafunzi wa mwalimu Majisifu wanatafuta haki ya kufunzwa vyema baada ya Mwalimu wao kutohudhuria shule kwa muda mrefu. Yusufu anatafuta haki baada ya kusingiziwa kumwuua Chichiri Hamadi.*
- *Raia wa Sokomoko wanatafuta haki dhidi ya Nasaba Bora anayewapokonya ardhi, mali, mabiruti na wake wao.*
- *Wafungwa wanatafuta haki kwa kukosa kufikishwa mahakamani.*
- *Waandishi wengi chipukizi kama Amani wanatafuta haki ya kazi zao baada ya kuibiwa miswada yao na akina Majisifu.*

## *TAMTHILIA*

### *SEHEMU C: TAMTBILIA*

T. Arege: *Mstahiki Meya*

*Jibu swali la 4 aula 54. "Anwani Mstahiki Meya ni kinaya." Jadili ukweli wa kauli hii kwa kurejelea tamthilia. (Alama 20)Anwani Mstahiki Meya ni kinaya kw vile anayeitwa Mstahiki anatakiwa kuwa mtu wa kuheshimiwa. Kama kiongozi heshima hutokana na uongozi bora unaowafanya raia kuonea fahari uongozi wa kiongizi wao. Hata hivyo, Mstahiki Meya hakustahiki kuitwa kiongozi kwa sababu zifuatazo:*

- *Wafanyakazi wa mji wanaendelea kufanya kazi kwa muda mrefu bila mshahara.Hospitali hazina dawa na wagonjwa wanakufa kutokana na magonjwa yanayoweza kutibiwa kwa urahisi,*
- *Kuna njaa kiasi kwamba wafanya kazi wake wanakula mabaki ya chakula kutoka nyumbani mwake na kuugua.*
- *Anapanga na Bili jinsi wataipunja baraza kupitia kesi ya mwenye kandarasi anayedai haki yake.*
- *Anadanganya kuwa ameagiza dawa kutoka ng'ambo huku akijua fika kuwa hajaagiza.*
- *Anawatenga wanaodhamiria kumsaidia kuongoza vizuri kama vile Siki na Diwani III.*
- *Anaharibu aasasi za serikali kama vile hospitali huku mkewe akienda ng'ambo kujifungua.*
- *Anawaita viongozi wa wafanya kazi ofisini mwake akijua kuwa hakuwa na mpango wa kushughulikia malalamiko yao.*

- *Badala ya kusuluhisha matatizo yanayokumba mji wa Cheneo kwa majadiliano, anaamua kutumia vyombo vya utawala kunyamazisha upinzani.*
- *Ananyakua ardhi ya umma na kujigawia pamoja na marafiki zake hasa Bili.*
- *Anaidhinisha kutotozwa kodi kwa madiwani huku wafanya kazi wa kawaida wakilazimishwa kufanya kazi kwa miezi mingi bila mshahara kutokanan na nakisi ya kifedha.*
- *Anashiriki katika wizi wa fimbo ya Meya ishara ya mamlaka ya cheo chake.*
- *Anaingilia mambo yasiyo na maana yoyote kama vile ukubwa wa mayai aliyopikiwa badala ya kushughulikia matatizo katika Cheneo kwa busara ifaayo.*
- *Anakiri kudanganywa na Bili na kuwategemea madiwani ambao hawakuwa na ujuzi wa kutosha.*
- *Anawahonga madiwani ili wamuunge mkono badala ya kuwatambua kama wawakilishi wa wananchi watakaompa ukweli wa mambo ili kuongoza anavyostahili.*
- *Anamhonga mhubiri ili aendelee kumwombea yeye badala ya kubadili uongozi wake unaoendelea kuzorotesha hali mjini Cheneo.*
- *Anaendelea kumlipa Bili kwa huduma isiyo na manufaa yoyote. Bili alijua kuwa alikuwa akimdanganya Meya na mambo yanapoharibika anatoroka pasipo kwaheri.*
- *Anapogundua alidanganywa mambo yalikuwa yameharibika kiasi cha kutobadilika.*
- *Anahakikisha kuwa masiahi ya kiafya ya wenye mamlaka yameshughulikiwa huku raia wake wakugua na kufa kwa ukosefu wa huduma hospitalini.*
- *Anautambua urafiki wa kusifiwa zaidi ya utaaiamu. Diwani III na Siki hawakutambuliwa kwa vile katika kumwmbia Meya ukweli walionekanan kama maadui wake,*
- *Anakosa kufikiria na kufanya maamuzi huru na kutokana na haya anadanganywa na waliojali masilahi yao kama Bili na Diwani ! na Diwani II.*

5. *"... dawa ya adui ni kummegea unachokula."*

**(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (Alama 4)**

- *Anayesema maneno haya ni Bili akimwambia Mstahiki Meya. Wamo ofistni mwake Mstahki Meya. Walikuwa wakizugumza kuhusu mwanakandarasi aliyekuwa ameshtaki Baraza akidai pesa zake.*

**(b) Jadili jinsi dawa inayorejelewa inavyozorotesha hali katika mji wa Cheneo. (Alama 16)**

- *Dawa inayorejelewa ni ufisadi. Ufisadi umezorotesha hali katika Cheneo kwa njia mbalimbali kama:*
- *Meya anaidhinisha kuongezewa mishahara kwa madiwani ili wamuunge mkono. Hazina ya baraza inamomonyoka zaidi. Madiwani hawampi ushauri wa kweli na uongozi unaanguka.*
- *Meya anamgawia Bili viwanja vinne. Bili anaishia kumpa ushauri wa kuporosha. Meya anaifisidi hazina ya baraza kwa kumpeleka Bili na familia yake kwa burudani.*
- *Meya anaunda kamati nyingi ili kuwahonga madiwani wanaomuunga mkono. Anaishia kushauriwa kufanya maamuzi yasiyo ya busara, anakataa kuwasikiliza wafanya kazi, mji umejaa urundo, wageni wanakosa kufika na uongozi wa Meya unaanguka.*
- *Meya anamlipa Bili kwa huduma ambayo kwa ukweli hajatoa. Huu unakuwa mzigo kwa hazina ya baraza.*
- *Meya anaidhinisha Diwani I na Diwani II kulipwa 'overtime' na hali hawajafanya lolote. Anaishia kumpa Bili upenyu wa kushauri wauze fimbo ya Meya.*
- *Meya anaidhinisha kutotozwa kodi kwa madiwani kwa kutaka wamuunge mkono. Hili linalinyima baraza pato na kuzidisha nakisi ya fedha.*
- *Meya anamhonga mhubiri kwa sadaka ili aendelee kumwombea. Mhubiri anashindwa kumkosoa Meya, uongozi unaanguka.*
- *Bili anamshauri Meya amwambie mwanakandarasi alishtaki baraza ili apewe fidia kwa kukatizwa kwa kandarasi. Meya anapata fungu lake pia.*
- *Raia wanachukua hongo kutoka kwa viongozi. Wanawachagua na kuendeleza uongozi mbaya. Meya anamwambia Siki kuwa hata akitaka uongozi mara nne, tano na sita atapewa kwani ana akili na uwezo wa ushawishi.*
- *Ufisadi unamfanya Meya kumshirikisha Bili katika maamuzi muhimu ya Baraza, na hali Bili si mfanya kazi wa Baraza. Bili anaishia kumporosha Meya.*
- *Ufisadi unamfanya Diwani I (Bwana Usalama) kufanikisha wizi wa fimbo ya Meya. Anatoka nayo kasha anatangaza kwamba kulitokea rabsha ikaibwa.*
- *Ufisadi unamfanya Meya, Diwani 1, Diwani II na Bili kutotoa siri kuhusu nyama ya kuiba fimbo ya Meya linapata hasara.*

## SEHEMU D: USHAIRI *Jibu swali la 6 aula 7*

***6. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.***

**Kilio cha Lugha**

*Ni wimbo najiimbia, nijiliwaze*
*Sina wa kusaidia, **nasongwa** sina nafasi*
*Kiwa kwetu naumia, kwengine si mahususi*
*Lugha ya mtu mweusi, Kiswahili chalilia*

*Wataalamu ni nani, mulipo mwaninyanyasa*
*Hamna nami imani, wala kupanga siasa,*
*Mwasema sayansini, siku ningalitosa,*
*Mwanambia nikotosa, kuiva sijafika.*

*Ela muelewe sana, Maamuma na Imamu,*
*Mulipokuwa vijana, kwenu nilikuwa timamu,*
*Sasa mumesoma sana, mwaniona ni haramu,*
*Mujue kuwa dawamu, utumwa mwauridhia.*

*Mzaliwapo mwalia, 'maa', maneno ya kwanza,*
*Lugha munayokulia, ya mama zetu ya kwanza,*
*Wa lugha muwedoria, muweze na kuikuza,*
*Sio kujipendekeza, uzungu kuigiza.*

*Majira ya ukoloni, ukombozi kusambaza,*
*Lugha mulithamini, Kiswahili kufukiza,*
*Hata kule risavuni, kizungu hanikuwaza,*
*Sasa mbona mwanibeza, mbali mwanitupilia?*

*Sayansi sio asili, msamiatiwe sinao,*
*Sayansi yataka mbali, msamiati ni wa hao*
*Nitakuwa Kiswahili, kiomba majina yao*
*Lugha kujikuza kwao, huomba linalofaa.*

*Enyi viongozi wetu ipangeni nadharia,*
*Kujenga siasa yetu, tuzidi kuwa huria*
*Lugha hata 'mbusha watu, tuche **kuriaria,***
*Sifa ni kwa chake mtu, cha mwenzi hutoringia.*

*Utajiri wangu hasa, nikiwatajia wote,*
*Msamiati huwa, ni wa Afrika yote,*
*Na methali za kuasa, nahau na ngeli zote,*
*Na nisemwapo popote, ujumbe hukamilika.*

*Afrika ndipo petu, pa wabantu halisi,*
*Baba na mama ni Bantu, shina la wangu ukwasi,*
*Warabu na wengi wetu, sio wangu **Adinasi***
*Kwao 'meomba kiasi, ili kujizidisha.*

*Mfumo mpya hongera, wa elimu humu Kenya,*
*Lugha takuwa imara, ukabila tutafinya,*
*Kiswahili ni ibara, kila mtu kiimanya,*
*Methali imetuonya, mtumwa si mwasilia*

*Tamati lugha yalia, yabaguliwa bayana,*
*Kukua imeridhia, msamiati kufana,*
*Wengine wataijulia, kwa marefu na mapana,*
*Lugha yenu ya maana, mwaipuuza yalia.*

**(a) Shairi hili ni la aina gani? Toa sababu. (Alama 2)**

- *Tarbia - mishororo mine katika kila mshororo.*

**(b) Kwa kutoa hoja ime, eleza kwa nini shairi hili likaitwa kilio cha lugha. (Alama 4)**

- *Kiswahili chapuuzwa kuwa hakijakomma*
- *Waliosoma hawakienzi Kiswahili wakifikiria hawana haja na lugha hii.*
- *Viongozi hawakienzi Kiswahili katika kujenga siasa.*
- *Kiswahili hakipewi nafasi.*
- *Waafrika hawaoni utajiri wa Kiswahili kuwa na msamiati kutoka aarika nzima.*

**(c) Andika ubeti wa tatu kwa lugha ya nathari. (Alama 4)**

- *Kila mmoja aelewe*
- *Mlipokuwa vijana mlikitumia Kiswahili.*
- *Baada ya kusoma mmeanza kukidharau*
- *Kwa kufanya hivi mjue mwafurahia utumwa.*

**(d) Eleza toni ya shairi hili. (Alama 2)**

- *Toni ya huzuni - lugha ya mtu mweusi chalia.*

**(e) Tambua uhuru wa kishairi uliotumiwa kwa kurejelea mifano milatu. (Alama 3)**

- *Inkisari - kiwa - nikiwa*
- *Mazida - muelewe - mwelewe*
- *Tabdila - mulithamini - mlithamini.*
- *Kuboronga lugha - hamna name imani - hamna imani name.*
- *Utuhozi - risaruni.*

**(f) Bainisha nafsineni katika shairi. (Alama 2)**

*Hafsheni*

- *Mtetezi wa lugha ya Kiswahili anayelalamikia kupuuzwa kwa Kiswahili.*
- *Aliyezinduka na kutambua umuhimu wa Kiswahili barni Afrika.*

**(g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kwa mujibu wa shairi. (Alama 3)**

***(i) nasongwa***

- Nasagwa – naumia

***(ii) kuriaria***

- kuzurura, kurandaranda

***(iii) adinasi***

- binadamu

**7. *Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.***

**T. Arege:** *Barabara*

*Barabara bado ni ndefu*
*Nami tayari nimechoka tiki*
*Natamani kuketi*
*Ninyooshe misuli*
*Nituliza akili.*

*Lakini*

*Azma yanisukuma*
*Mbele ikinihimiza kuendelea*
*Baada ya miinuko na* ***kuruha***
*Sasa naona unyoofu wake*
*Unyoofu ambao unatisha zaidi.*

*Punde natumbukia katika shimo*
*Nahitaji siha zaidi ili kupanda tena*
*Ghafla nakumbuka ilivyosema*
*lie sauti zamani kidogo*
*"Kuwa tayari kupanda na kushuka*

*Ingawa nimechoka*
*Jambo moja li dhahiri*
*Lazima nifuate barabara*
*Ingawa machweo yaingia*
*Nizame na kuibuka*
*Nipande na kushuka.*

*Jambo moja nakukumbukia:*
*Mungu Je, nimwombe tena?*
*Hadi lini? Labda amechoshwa na ombaomba zangu*
*Nashangaa tena!*

*Kitu kimoja nakiamini*
*Lazima niendelee kijitahidi kwa kila hatua mpya*
*Nijikokote kuiandama hii* ***barabara yenye ukungu***
*Nikinaswa na kujinasua*
*Yumkini nitafika mwisho wake*
*Ingawa wangu mwisho haitauwahi kabla.*

*(a)* **Eleza toni ya shairi hili. (Aiama 2)**

- *Toni ya mahimaini - lazima niendelee kujitahidi kwa kila hatua.*
- *Toni ya uchovu - Nami tayari nimechoka tiki.*

**(b) Mshairi ana maana gani anaposema "Kuwa tayari kupanda na kushuka" katika ubeti wa tatu? (Alama 2)**

- *Kuwa tayari kukabiliana na uzuru na ugumu wa maisha*

**(c) Fafanua tamathali tano za usemi zilizotumiwa katika shairi hili ukizitolea mifano mwafaka. (Alama 10)**

- *Taswira - picha inayojitokeza unaposoma kazi ya fasihi n.k. wa miinuko na kuruba.*
- *Taswira kinzani - Nizame na kuibuika*
- *Nipande na kushuka.*
- *Taashira - Barabara kuimarisha maisha.*
- *Mswali balagha - hadi lini?*
- *Uzungumzi nafsi - mizame na kuibuka, -Nipanda na kushuka.*

**(d) Eleza ujumbe unaojitokeza katika ubeti wa tano wa shairi hili. (Alama 2)**

- *Msemaji ameshangaa kuwa amekuwa akiomba kwa muda na anatilia shaka iwapo Mungu amechoshwa na maombi yake.*

**(e) Eleza maana ya: (Alama 2)**

***(i) kuruba***

- *Hali ya kuwa na vikwazo na magumu ya maisha.*

***(ii) barabara yenye ukungu***

- *Mkondo wa maisha ambapo anayokubaliana nayo mja si wazi. Kila hisia huibua mambo mapya.*

## 8.SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

## 2016

**(a)Kwa kutumia mifano mwafaka eleza majukumu matano ya nyimbo katika jamii.(Alama 10)**

- *Nyimbo huhifadhi historia ya jamii. Mfano nyimbo za siasa, nyimbo za sifa, nyimbo za vita.*
- *Huhifadhi na kupitisha utamaduni k.v mbolezi hubeba utamaduni wa jamii kuhusu kifo.*
- *Huliwaza kv. Mboiozi Kuonyesha ustadi/ubora wa jamii.*
- *Huhamasisha*
- *Hudimisha*
- *Kukuza utangamano*
- *Ni njia ya kutakwa hisia*
- *Huadilisha.*
- *Kukashifu tabia hasi*
- *Kusifu tabia chanya*
- *Hukuza uzalendo kuimarisha ubunifu.*

**(b) Ili kuweza kufanikisha uwasilishaji wa utanzu wa nyimbo kwa hadhira eleza mambo anayohitaji mwimbaji. (Alama 10)**

- *Kuwa na sauti ya kurutia*
- *Kuihusisha hadhira*
- *Kuieiewa hadhira*
- *Kuelewa utamaduni wa hadhira*
- *Kutumia viziada lugha*
- *Kuwa mkakamavu*
- *Aelewe lugha ya hadhira*
- *Awe mbunifu*
- *Ahusishe masuala ibuka yanayoathiri jamii ili kupitisha maadili yafaayo.*
- *Awe na kumbukumbu nzuri.*
- *Avae maleba*
- *Abadilishetoni kulingana na ujumbe*
- *Kutumia ala kwa njia mwafaka ili kukuza mvuto wa utungo wake.*

## ***HADITHI FUPI***

**K. Walibora** na **S. A. Mohamed:**
*Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine 1.*
***Lazima***

**Jadili maudhui ya elimu kwa mujibu wa "Kanda la Usufi", "Shaka ya Mambo" na "Tazama na Mauti", (Alama 20)**

- *Shule imesawiriwa kama mahali pa kuadilisha wanafunzi.*
- *Kuhakikisha kuwa wanafunzi wamo katika hali nzuri ya kiafya ili kuendeiea katika masomo -mfano - desturi ya shule ya Askofu Timotheo kuwachunguza wasichana wote kama wana mimba.*
- *Matokeo ya vitendo vya wanafunzi yanadhihirika katika hadithi tofauti. Katika Kanda la Usufi, Sela na Masazu hawafanyi vyema kwenye mtihani*
- *Katika Tazamana na Mauti, ukosefu wa hamu ya masomo unamfanya Lucy asifanye vyema kwenye mtihani.*
- *Wazazi hukatatam-aa watoto wao wanapoenda kinyume na matarajio yao.*
- *Elimu pia humpa binadamu uhuru kujipangia mustakabadhi wake.*
- *Masazu anapata kazi ya kijungu jiko huku Sela akitamani kumchukua mtoto wake ajilele kwa vile hakuwa na la kufanya Masazu anapoenda kazini*
- *Katika Kanda la Usufi imeelezwa kuwa wasichana walitarajiwa kuendeleza shughuli zao kwa utulivu na ustaarabu huku wakizingatia maadili ya hali ya juu. Elimu pia inatarajiwa kuwapa wanafunzi nafasi ya kukuza vipaji vyao na kuingiliana ili kuelewana zaidi.*
- *Jukumu la mwanafunzi katika masomo limejitokeleza Bi Margaret mwalimu mkuu wa shule ya Askofu Timotheo anapowahutubia wanafunzi na kusisitiza uwajibikaji katika vitendo vyao.*
- *Katika Tazamana na Mauti Lucy anaamini kuwa jiji hili lina raha kamili bila karaha.*
- *Anategemea mzungu atakayemwoa na kumpeleka London na baadaya kufika London akaanza kutegemea kifo cha Bw. Crusoe ambacho kingempa urithi na raha aliyotaka maishani*
- *Hili linadhihirika wakati mzee Butali anapomwuliza mwalimu kwa nini wazazi huwapeleka watoto shuleni.*
- *Ukosefu wa elimu umeonyeshwa kama mojawapo ya njia zinazowapa vijana mitazamo finyu kuhusu maisha.*
- *Esther katika Shaka ya Mambo alijua alichokuwa akitafuta.*
- *Kwa upande mwingine mustakabali wa Lucy ulitegemea wengine.*
- *Alikuwa amepanga ni kwa muda gani angeendelea kufanya kazi jinsi atakavyopanga wakati wake baada ya kujiunga na chuo kikuu na anachotaka kusomea.*